HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG

SHULE YA SEKONDARI DANIEL NOUD

S.L.P 242,

KATESH- HANANG.

TAREHE ……...

MOB: 07837360804

Kumb Na……

Jina la Mwanafunzi…….

S.L.P ……..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI DANIEL NOUD ILIYOKO WILAYA YA HANANG MKOA WA MANYARA MWAKA 2021

Utangulizi

Ninayofuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari ya Daniel Noud mwaka 2021.Muhula wa masomo utaanza tarehe 11.01.2021.Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11.01.2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 15.01.2021.

Kila mwanafunzi anatakiwa kuripoti katika tarehe iliyoelekezwa ili kuepuka KUPOTEZA nafasi yake na mzazi kuchukuliwa hatua za kisheria kwa kushindwa kumripotisha mwanafunzi kwa wakati.

1. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

   SARE ZA SHULE

   (a) WAVULANA

   - Suruali dark blue- upana 16 iwe na turn up
   - Shati nyeupe mikono mifupi
   - Sweta rangi ya dark blue
   - Tai rangi ya dark blue
   - Viatu vyeusi na visiwe na visigino virefu viwe na kamba
   - Soksi rangi nyeusi.s
   - Fulana nyeupe ya kuvalia ndani ya shati
   - Mkanda mweusi usiwe na kichwa kikubwa
   - Vifaa vya michezo: viatu vya michezo visivyoteleza na Soksi nyekundu,Tract suit nyekundu, Bukta nyekundu na Tisheti nyekundu

Angalizo:Suruali isiwe na upana chini ya 16 na ni marufuku kuvaa viatu vya plastiki kama sare ya shule.

(b) WASICHANA

- Vifaa vya michezo: viatu vya michezo visivyoteleza na Soksi nyekundu,Tract suit nyekundu, Bukta nyekundu na Tisheti nyekundu
- Sketi dark blue mshono wa rinda box
- Shati nyeupe mikono mifupi
- Sweta rangi ya dark blue
- Viatu vyeusi na visiwe na visigino virefu na viwe na kamba
- Soksi rangi nyeupe
- Fulana nyeupe ya kuvalia ndani ya shati jeupe

ANGALIZO: Sketi lazima ivuke goti marufuku kuvaa viatu vya plastic kama sare ya shule.

VIFAA VYA KUJIFUNZA

Daftari kubwa Counter Quire2 ziwe 10, kalamu, mkebe wa hesabu na kamusi ya kiingereza.

CHAKULA CHA WANAFUNZI

- Mwanafunzi aje na debe 1 na kilo 16 yaani kilo 36 za mahindi na maharage robo tatu ya debe yaani kilo 15 kwa muhula wa kwanza.
- Mwanafunzi aje na kiasi cha shilingi **22500/=** elfu ishirini na mbili na mia tano tu kwa muhula na kwa mwaka ni elfu arobaini na tano tu **45000/=** kwa ajili ya huduma za chakula fedha hizo zilipwe benki kupitia **Akaunti Na.41010006345** na jina la **Akaunti ni Kamati ya chakula Daniel Noud Sekondari.**
- Aje na sahani,bakuli na kijiko kwa ajili ya chakula (viwe vya bati) vitu vyote hivyo aje navyo siku ya kuripoti

2. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo inayotolewa na wizara ya elimu, mafunzo na sayansi na teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais- Tamisemi yenye jukumu na usimamizi wa elimu, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi:-

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi,wafanya kazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
(c) Kushiriki kuandaa maandalio ya jioni (preparation)
(d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyinginezo utakazopewa.
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo kwa muda wote wa uanafunzi wako katika shule.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
(i) Kutunza mali za shule.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUKUFUKUZISHA SHULE MOJA KWA MOJA

(a) Wizi

(b) Uasherati na ushoga

(c) Ubakaji

(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocaine mirungi,kucheza kamali kama vile kubeti n.k.

(e) Kupigana na kupiga.

(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

(g) Kudharau bendera ya Taifa.

(h) Kuwa mjamzito/kupata mimba/kusababisha mimba.

(i) Kuoa au kuolewa.

(j) Kutoa mimba.

(k) Kugoma, kuchochea na kuongeza au kushiriki vurugu na kuvunja amani na usalama wa shule au watu.

(l) Kukataa adhabu kwa makusudi

(m) Kuwa na simu ya mkononi.

MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA NA MWANAFUNZI.

(a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali na kukabidhiwa kwa mkuu wa shule atakaporipoti. Fomu imeambatanishwa.

(b) Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

Tafadhari soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE YA DANIEL NOUD SEKONDARI

…….

MKUU WA SHULE

FOMU NA 1

IJAZWE NA MGANGA MKUU/ WILAYA YA/KITUO CHA AFYA MWANAFUNZI AJE NAYO NA KUMPA MKUU WA SHULE (USIPIMWE KWINGINE KOKOTE)

Mimi (Jina la mganga mkuu wa mkoa/Wilaya/Kituo cha Afya…….
Ninathibitisha kuwa mwanafunzi huyu(jina la mwanafunzi……
Amepimwa nami kikamilifu na kuonekana kuwa **ana /hana** afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo.

HALI YA MWILI

1. Mapigo ya moyo……
2. Kiasi cha damu……
3. Kundi la damu……..…
4. Mkojo…….....
5. Kinyesi……
6. Macho……
7. Masikio……

TOA MAONI YAKO KWA KILA KIPENGELE TAJWA

A. MAGONJWA

a. Amewahi/anayo/hana magonjwa yafuatayo
b. Pumu……..……
c. Kifua kikuu……..……..
d. Kifafa……...…
e. Shinikizo la damu…….
f. Vidonda vya tumbo ……
g. Sickle cell……
h. Ukoma……
i. Maradhi ya zinaa……
j. Maradhi ya akili……
k. Maradhi mengine makali yasiyotajwa hapo juu……

ZINGATIA:Kujaza taarifa za uwongo zisizothibitishwa ni kosa la kisheria.

SAINI NA MHURI WA DAKTARI/MGANGA

……
Tarehe……